Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 81 No. 222 | RAM - SHAW. 1442 AH | MEI 2021 | HIJRAT 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na hakuna kitu kilichowazuia watu wasiamini na kuomba msamaha kutoka kwa Mola wao mwongozo ulipowafikia, isipokuwa kwamba walichagua kufuata njia ya watu wa zamani pamoja na yale yale yaliyowasibu, au waliisubiri adhabu ya Allah iwakumbe uso kwa uso. (Al-Kahf 18:56)

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad saw

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a.
Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

DHULMA KWA MTUME S.A.W.

Hata Mtume mwenyewe s.a.w. hakusalimika, alikuwa akipewa usumbufu wa aina mbali mbali. Siku moja alipokuwa akifanya ibada, watu wakamzingira nguo shingoni mwake na kuanza kuivuta kiasi ya kwamba macho yote yakamtoka pima. Mara akaja Hadhrat Abu Bakar r.a. na kumuokoa katika hali ile huku akiwaambia: Enyi watu! Mnamuua mtu kwa kosa hili tu kwamba yeye anasema kuwa Mungu ni Mola wangu?

Wakati fulani alikuwa anasali akiwa amesujudu yalipoletwa mautumbo ya ngamia na kuwekwa mgongoni kwake na kutokana na uzito wake alishindwa hata kuinua kichwa chake, hadi walipokuja baadhi ya watu na kuuondoa utumbo ule mgongoni kwake.

Wakati fulani alikuwa akipita mtaani, mara akazungukwa na kikundi fulani cha vijana wa kihuni wa hapo Makka na kumpiga piga makofi shingoni huku wakisema: Huyu ndiye yule mtu anayesema; Mimi ni nabii!



Mara kwa mara mawe yalikuwa yakivurumishwa nyumbani kwake kutoka kwenye nyumba zilizomzunguka. Vitu vichafu vilikuwa vikitupwa jikoni mwake, vilivyojumuisha mautumbo ya mbuzi na ngamia. Alipokuwa akisali alikuwa akimwagiwa vumbi kiasi ya kwamba akalazimika kusali kwa kujificha chini ya jiwe lililotokeza toka kwenye mwamba. Lakini dhulma hizi hazikupotea bure. Watu wenye asili ya wema walikuwa wakiziona na mioyo yao ikawa inavutika kwenye Islam. Siku moja Mtume s.a.w. alikuwa ameketi juu ya kilima cha Swafaa karibu na nyumba ya Kaaba wakati Abu Jahal, aliyekuwa Kiongozi wa watu wa Makka na adui yake mkubwa, alipopita maeneo hayo na kuanza kummiminia matusi mabaya mno, Mtume s.a.w. aliendelea kuyasikiliza matusi yale bila ya kusema chochote. Alisimama kimya na kuelekea nyumbani kwake. Mtumishi fulani wa kike aliyetumika katika ukoo wake alikuwa akiliona tukio hili.

Wakati wa jioni, baba mdogo wa Mtume s.a.w., Hamza r.a., aliyekuwa mtu shujaa sana aliyeogopwa na watu wote kutokana na ushujaa wake, alirudi kutoka mawindoni huko msituni na kuingia nyumbani mwake kwa fahari, akiwa ameuning'iniza upinde wake begani. Moyo wa kijakazi yule ulikuwa umeathirika mno na mandhari ya tukio lile la asubuhi. Alishindwa kujizuia alipomuona Hamza katika hali ile na akamkejeli kwa kumwambia: Wewe wajiona shujaa sana ukipita na silaha kila wakati, lakini wafahamu kuwa Abu Jahal alimtendeaje mwana wa nduguyo leo asubuhi? Hamza akauliza: alifanya nini? Akamuhadithia Hamza tukio lote lile.

Ingawa Hamza hakuwa mwislamu, lakini alikuwa ni mtu mwenye moyo mwema. Habari za Islam alikuwa ameshazisikia na kwa yakini moyo wake ulikuwa umeshavutika, lakini kutokana na shughuli zake za maisha za hapa na pale, hakuweza kupata

Endelea uk. 2

Mwamini Mungu Si Mtovu

Na **Miye**

Hivi punde tumeishiliza kufunga Swaumu ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. lbada hii ni maarufu katika takribani dini nyingi ijapokuwa kanuni zimekhitilafiana. Naam, Swaumu aliyofunga **Sayidina Mussa A.S** kabla hajapata amri kumi, hata Swaumu aliyotekeleza **Nabii lssa A.S** kabla hajapewa shughuli za utume ni tofauti na maagizo aliyoyatoa kwa wafuasi wake. Wapo watu waliofunga siku **3** na kumi, wengine siku **40** hadi **50**, wengine wao walifunga Swaumu muda wote wa siku za maisha yao.

Quran Tukufu kwenye ibada hii ya Swaumu inaeleza hivi *"Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Swaumu kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu kwa siku zilizohesabiwa. Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine, Na wale wanaoweza, watowe fidia kwa kumlisha maskini. Na atakayefanya wema kwa radhi ya nafsi yake, basi ni bora kwake, na kama mkifunga ni bora kwenu ikiwa mnajua"*. (**Sura Albaqara aya 184 hadi 185**)

Endelea uk. 3



KUMRADHI

Tunaomba radhi kwa makosa ya uandishi katika toleo la Jan-Feb kwa makala zinazohusu Jamia Ahmadiyya Tanzania iliyopo Morogoro kuweka jina la muandishi wa makala hizo kuwa Juma Iddy Abedi ambaye siye aliyeandika. Tutajitahidi kuondoa kasoro hizo kwa siku zijazo. InshaAllah

Buriani Mwakitalima, Tutakukumbuka uk. 10

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SISI NI WA ALLAH

Jumuiya ya Ahmadiyya Afrika Mashariki iko katika majonzi makubwa ya kuondokewa na Naibu Amir Tanzania, Shujaa na mpenzi wa mahubiri, Mwenye roho ya huruma na mapenzi kwa masikini, mtafutaji elimu, Isa Mwakitalima aliyeaga dunia katika hospitali kuu ya Muhimbili tarehe 25 Mei 2021 na kuzikwa makaburi ya Ahmadiyya Wailesi Temeke tarehe 26 Mei 2021. Sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Maisha ya Isa Mwakitalima *sahib* yametuachia mambo ambayo yanaweza kutusaidia kufanya maisha yetu yawe bora zaidi. Nsekela Mwakitalima alipoingia katika Islam alichagua jina la Isa. Nabii Isa a.s. alikuwa Nabii wa Allah aliyefundisha Umoja wa Allah, kuwapenda masikini, kuwa na huruma. Jina kama vilivyo vyakula lina athari kwa binadamu. Ndio maana Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alihimiza tuwape watoto wetu majina mazuri. Na Waahmadiyya wamelielewa somo hili kwa kumuandikia Khalifatul Masih a.t.b.a. ili awachagulie majina ya watoto wao. Wahaya wana methali - *eibala libi litala nyinalyo* – "Jina baya humuangamiza mwenye jina". **Tuwape watoto wetu majina mazuri**.

Utamaduni wa kusoma umepungua sana. Vitabu vya kutosha tunavyo katika Kiswahili na Kiingereza. Pindi alipojiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya Isa Mwakitalima *sahib* alifunga urafiki na kutafuta elimu. Alisoma vitabu na kufanya bidii kujifunza Qur'an Tukufu na Kiingereza ili asome vitabu vingi vya Jumuiya ambavyo vimo katika lugha ya Kiingereza. Mapenzi yake ya elimu yalimpelekea kuwasaidia waliokuwa wanatafuta elimu. **Utamaduni huu wa kusoma na kutafuta elimu ni utamaduni wa maendeleo**.

Isa Mwakitalima *sahib* alitanguliza dini mbele ya kila kitu. Yeye alikwenda maili moja zaidi. Sio kutanguliza dini tu kwa maneno bali kwa vitendo. Wapi penye shughuli za Jamaat na usimkute Isa Mwakitalima *sahib*? Kwenye mahubiri Kariakoo, Mjadala Nguruka, Jalsa Salana London, Nairobi, Kampala, utamkuta. **Kutanguliza dini kwa vitendo** ni somo ametuachia.

Mwaminio hatakiwi kuwa kisiwa. Anatakiwa atoke achanganyike na watu. Ajue wanachosema. Wanachofikiri. Anajenga marafiki na hiyo ndio njia nzuri ya kuvuta watu. Unafuata huko waliko. Mnafahamiana na unawapa msimamo. Isa Mwakitalima *sahib* alikuwa mpenzi wa kabumbu. Kwenye mpira kuna mengi ya kujifunza. Kwanza kukaa chini na kuwa na wazo la kuwa timu. Hilo ni jambo jema. Timu hiyo inajenga ushirikiano, kusaidiana. Lakini mnachagua viongozi. Kwa hiyo mnapata uzoefu wa demokrasia. Mpira unaibua kipaji cha mtu mmoja na vipaji vyenu nyote kwa ujumla. Lazima mshirikiane. Bila kushirikiana hakuna mafanikio. Nyote mna shabaha moja- kufunga goli. Mashabiki wameungana pamoja wanataka ushindi. Kwa jicho la hekima kila tukifanyacho kina faida na hekima.

Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alijiunga na chama cha kutetea wanyonge. Alihudhuria kwenye michezo. Kila ukurasa wa maisha yake una somo kwetu. **Tujitahidi kufungua kurasa za maisha yake** kama alivyojitahidi kufanya Isa Mwakitalima *sahib*. Tunatakiwa tujifunze. Tujiunge na vyama vya kisiasa na kijamii. Na huku **tupeleke nuru ya Ahmadiyya**. Tutoke ndani kama alivyofanya Naibu Amir *sahib* na **tubadili kila tunachokifanya yawe mahubiri na mfano kwa wengine**.

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*

Kutoka uk. 1

fursa ya kutafakari kwa kina, lakini alipolisikia tukio hilo akapandwa na jadhba. Pazia ya mghafiliko ikamtoka machoni na akafahamu kwamba sasa kitu chenye thamani ki hatarini kupotea. Wakati huo huo akatoka nje ya nyumba yake na kuelekea kwenye nyumba ya Kaaba iliyokuwa sehemu makhsus ya kukusanyikia na kushauriana ya viongozi wa Makka. Aliutoa upinde wake begani na kumpiga nao Abu Jahal kwa nguvu sana na kumwambia: Sikiliza! Hata mimi najiunga na dini ya Muhammad s.a.w. Asubuhi umemtukana bila sababu kwa kuwa yeye si mwenye kujibu. Kama wewe ni shujaa basi jibu kipigo changu. Tukio hili lilitokea kwa ghafla bila ya kutarajiwa kiasi ya kwamba hata Abu Jahal akashikwa na hofu. Waliokuwa pamoja naye wakasimama kutaka kupigana na Hamza. Lakini Abu Jahal alipotafakari kuhusiana na ushujaa wa Hamza na malipizo ya kabila lake, basi akawaza kuwa kama mapigano yangeanza basi matokeo yake yangekuwa ya hatari mno. Hivyo akachukua tahadhari kwa kuwazuia wenzake akiwaambia: Acheni! Kwa hakika nilimtukana vibaya mtoto wa nduguye.

UJUMBE WA ISLAM

Upinzani uliposhitadi, na huku Mtume s.a.w. na maswahaba wake wakiwa wameanza, kwa nguvu sana, kuwafikishia watu wa Makka ujumbe huu wa Mwenyezi Mungu, kwamba Muumbaji wa dunia hii ni Mungu Mmoja tu na hakuna mwabudiwa mwingine yeyote, Mitume wote waliopita walikuwa wakiukiri umoja Wake na walikuwa wakiwaita watu wao kwenye fundisho hili hili, hivyo mwaminini Mungu Mmoja na muachane na hiyo miungu ya (kuchongwa kwa) mawe isiyo na faida wala nguvu yoyote.

Enyi watu wa Makka! Hivi hamuoni kwamba kile kiwekwacho mbele yao, kama nzi watue juu yao, wao wanakuwa hawana uwezo hata wa kuwafukuza nzi hao? Hawawezi hata kujilinda kama yeyote awashambulie. Kama yeyote awaulize hawawezi kumjibu. Kama yeyote awaombe msaada hawawezi kumsaidia. Lakini Mungu Aliye Mmoja hutimiza mahitaji ya waombaji, Huwajibu wanaouliza, Huwasaidia wanaoomba msaada, na Huwakandamiza maadui Zake na Huwapa maendeleo ya juu waja Wake wenye kuabudu. Nuru huja kutoka Kwake inayoangaza kwenye mioyo ya wenye kumuabudu.

Sasa kwa nini mnamuacha Mungu wa aina hiyo na kuupoteza umri wenu kwa kuyainamia masanamu hayo yasiyo na uhai? Hivyo hamuoni kwamba kwa kuuacha Umoja wa Mwenyezi Mungu hata mawazo yenu yamekuwa machafu na mioyo pia imekuwa ya giza? Mmejiingiza katika mafundisho mbalimbali ya kuwazika tu. Hamtofautishi vilivyo halali na vilivyo haramu. Hamuwezi kupambanua vilivyo vizuri na viovu. Mnawadhalilisha mama zenu. Mnawadhulumu dada zenu na binti zenu na kutowapa haki zao. Hamuwatendei vizuri wake zenu. Mnazipora haki za mayatima na kuwatendea vibaya wajane. Mnawadhulumu masikini na wanyonge na mnazipora haki za wengine kwa kutaka kuuendeleza ukubwa wenu. Hamuuonei haya uwongo na udanganyifu. Hamuuchukii wizi wala ujambazi. Kamari na unywaji pombe imekuwa ndio shughuli yenu. Hamjali kuipata elimu wala kulihudumia Taifa. Hadi lini mtaendelea kughafilika juu ya Mungu Mmoja?

Njooni mjirekebishe na muwache dhulma. Kila mwenye haki mpatieni haki yake. Kama Mungu Ametoa mali, basi itumieni kwa kuihudumia nchi na watu na kwa maendeleo ya wanyonge na walio masikini. Waheshimuni wanawake na kuwapa haki zao. Wafahamuni mayatima kuwa ni amana ya Mwenyezi Mungu na mfahamu kwamba kuwatunza ni wema wa daraja la juu. Kuweni walinzi wa wajane. Stawisheni wema na ucha Mungu. Sio tu kutenda wema na uadilifu, bali muufanye mwenendo wenu kuwa wa kufanya na hisani. Hampaswi kufahamu kuja kwenu hapa duniani hakuna maana yoyote. Acheni nyuma yenu athari nzuri ili ipandwe mbegu ya wema wa milele. Heshima ya asili haiko kwenye kupokea haki bali kwenye kujitolea (kwa hali na mali).

Kwa hiyo jitoleeni Kurbani, kuweni karibu na Mwenyezi Mungu, onyesheni mfano wa kujitolea mbele ya watu wa Mwenyezi Mungu ili haki yenu istawi kwa Mwenyezi Mungu. Bila shaka sisi ni watawala, lakini msiutazame udhaifu wetu, uamuzi wa utawala wa ukweli umeshafanyika mbinguni. Sasa kipimo cha uadilifu kitawekwa kwa kupitia Mtume Muhammad s.a.w. na utawala wa haki na huruma utastawishwa ambamo hakuna yeyote atakayedhulumiwa, masuala ya dini hayataingiliwa, dhulma wanazofanyiwa wanawake na watoto zitafutwa na utawala wa Mungu Mmoja utastawishwa kwenye nafasi ya utawala wa Shetani.

MASHITAKA YA MAKAFIRI WA MAKKA KWA ABU TWALIB NA UIMARA WA MTUME S.A.W.

Itaendelea toleo lijalo

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Mwamini Mungu Si Mtovu

Kutoka uk. 1

Miye hivi sasa nina umri wa miaka **85**, ni mzee, macho yangu hayaoni vyema, kichwa changu kimetapakaa mvi kipato changu si kikubwa
kwa vile. Mimi si mkulima, si mfanya biashara wala si mfanya kazi. Kipato changu cha aduadu. Katika hali kama hii nilifikiria sana
nitatekelezaje ibada hii adhimu ya Swaumu, Nilijipa moyo kuwa nitafunga mimi na wale walo pamoja nami.
Mke wangu aliniuliza tutafungaje mwaka huu na hali ndani hatuna chochote cha maana. Nilimjibu kwa kumwambia kuwa tumtegemee
Allah na mwamini Mungu siku zote si mtovu. Sababu tulizonazo haitufanyi wala haitupi ruhusa ya sisi tusifunge Swaumu. Hatuumwi
wala hatumo kwenye safari, lnshaalah tutafunga Swaumu, Mungu Akipenda.

BARAKA YA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI.

Mwezi ulipoandama, siku ya kwanza Alhamdulilahl futari tulipata, lakini daku ikawa shida. Siku ya pili tukaendelea kufunga kama kawaida.
Hapajapita siku nyingi sana ninapokea simu "Assalam



alaykum. Mimi fulani hapa nina mzigo wako kutoka kwa bwana fulani nao umepitishwa kwa bwana fulani. Njoo uchukue". Mzigo huo kutoka kwa yule aliyeuchukuwa hadi kufika mikononi mwangu umepita kwa watu wawili tu. Naam, nikapokea furushi hilo. Nikafungua ndanimwe nikakuta Maharage, Ngano, Sukari, Tambi na Majani ya Chai. Kisha yule bwana akaingiza mkono wake wa kulia kwenye mfuko wo shati na kunikabidhi okali ya kitu ikiwa katika jamii ya fulushi hilo **Alhamdulilahi**.
Baada ya siku kumi hivi ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, alifika nyumbani kwangu bwana fulani, lakini hatukukutana sura kwa macho, bali aliacha hapa nyumbani bahasha yenye jina langu, Niliporudi kutoka kwenye mizunguko yangu, Mamie mwali akanikabidhi bahasha hiyo na kusema inatoka kwa Fulani na ameleta bwana Fulani. Nikaifungua ndani nikakuta kuna karatasi iliyokunjwa mora mbili, nikaikunjua. Nikaona nilichoona, **Jazakumullah**. Nikamuita mke wangu, njoo nawe uone kilichomo ndani ya bahasha ile uliyonipa.
Alipoona akatabasamu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Siku ya pili yote tukaletewa sukari **kilo 5** kutoka kwa ndugu yetu Fulani mwingine.
Neema hii kutoka kwa Allah ilitosha sisi kufunga Mwezi wa Ramadhani bila hofu wala wasiwasi, Alhamdulilahi, tuliweza kula futari nzuri daku ya kutosha hadi Mwezi kwisha. Miye na mke wangu tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. Lakini tumeambiwa asiyewashukuru watu
hamshukuru Mola. Kwa hakika tunawashukuru sana wale wote waliosababisha sisi tufunge Swaumu ya Mwezi wa Ramadhani mwaka huu bila matatizo yoyote. Allah awalipeni mema, awanyoosheeni mambo yenu yote, Amiin thuma Amiin.

TUSIPUUZE KUMUOMBA ALLAH.

Kabla sijaishiliza maandiko yangu haya, niseme kitu kimoja kwamba kwa hakika Mwenyezi Mungu Hayupo mbali na waja wake kamwe.
Yupo nasi karibu mno, " Na watu wangu watakapokuuliza juu yangu, basi hakika Mimi Nipo karibu. Nayaitika maombi ya mwombaji anaponiomba, basi waniitikie na waniamini ili wapate kuongoka" (Qur-an Tukufu sura, Albaqara aya ya **187**) Ni kweli, tena ni kweli tupu. Kwa hakika yule anayemtafuta Allah kwa mapenzi ya Taqwa na unyenyekevu mkubwa, hatokosa kupata rehema za Mungu na Baraka zake.

Wabillahi Tawfiq
KWAHERI

Mwongozo kwa ajili ya watoto wa Waqf e Nau

Hadhrat Khalifatul Masihi wa Tano*atba* akiwasisitiza Waqfin e Nau kujifunza lugha mbalimbali alisema katika hotuba yake ya tarehe 18 Juni 2004.

"***Mimi ninapenda kusema jambo moja kwa Waqfin e Nau, wale ambao tayari wameshafika umri wa kujitambua na wana nia na kipawa cha kujifunza lugha mbalimbali - hususani wasichana - wanatlojifunza Kiingereza, Kiurdu, Kiarabu au lugha nyingine basi yawapasa kubobea sana katika lugha hizi kiasi kwamba wajenge uwezo wa kutafsiri vitabu vya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. (Mimi niliwahi kushuhudia kwamba mara nyingi wasichana huwa wana kipawa cha kujifunza lugha vizuri). Hivi ndivyo tutakavyoweza kusambaza sehemu zote duniani."***

Agizo hili la Hadhrat Khalifa-tul-Masihi lifike kwa Waqfin-e-Nau wote kwa ajili ya utekelezaji.



Tarehe 25/05/2021, tumeondokewa na Ndugu Issa Mwakitalima na huku nyuma akituachia maumivu makubwa. Sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.
Ndugu Issa Mwakitalima alikuwa ni Naibu Amir (Utawala na Fedha) katika Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania.

إِنَّا لِلّٰهِ وَإِنَّـا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

Kabla hujaanza kujenga...

Anaandika **Mtaalamu Wetu**

Kwa kipind cha hivi karibuni, nimepata kazi zisizopungua 5 za watu waliojenga nyumba/ jengo wakagundua kasoro ktk ujenzi au plan au muonekano au ujenzi umekua wa gharama mno kuliko matarajio n.k na kunitaka niwafanyie redisign au renovation ya majengo yao. Ktk kesi takriban zote, kuna sababu ambazo zinakaribia kufanana nimezigundua, nimeona nishiriki nanyi mambo ya kuzingatia wakati unataka kujenga huenda ikamfaa mmoja wetu.

1. Utafiti

Kabla hujaanza kujenga unabid ufanye utafiti wa hali ya juu sana. Ongea na watu mbalimbali waliojenga, wataalam n.k ambao wameshajenga au ni wajenzi wakushauri juu ya wazo lako. Tembelea Internet kudodosa dodosa juu ya mambo kadha wa kadha ya ujenzi. Hii itakusaidia kuanza ujenzi ukiwa na picha kamili ya shughuli nzima.

2. Mchoro

Hapa ni sehemu nyeti sana ambapo watu wanapachukulia poa. Hapa unahitaji mtaalam wa kuchora. Kwenye mchoro usiangalie uzuri wa jengo tu, bali angalia pia bajeti, aina ya jengo na mazingira yako, mantiki ya plani ya jengo n.k

Kwenye kuchora ndio sehemu ya kufanya marekebisho, kufuta na kuchora tena. Chochote utakachoridhia kichorwe ndio



kitakachojengwa, ukichorewa jengo kubwa, utajengewa jengo kubwa maana lugha ya ujenzi ni michoro.

Bajeti: mchoraji anabidi akushauri sawa na bajeti yako. Ukichukua mkopo wa mil 50, ukachagua jengo zuri lenye square mita 200 na mchoraji akakuchorea bila kukushauri, utahamia kwenye hiyo nyumba na madirisha ya nyavu, haina aluminum panel, haijapigwa rangi nje na vitu kibao havijakamilika.

Aina ya jengo na mazingira yako teknolojia ya ujenzi inatofautiana baina ya sehemu na sehemu. Mfano kujenga jengo la matofali ya kuchoma Dar ni ngumu kuliko mikoani, ujenzi wa mawe Dar ni mgumu pia. Ujenzi wa hidden roof sio common Dar hivo kuna wataalam wachache wanaoweza kukupa kazi bora... hivi na vingine lazima vifikiriwe.

Mantiki ya plani ya jengo: hapa wengi wanakujaga kuvunja kuta wakiwa site. Kila ukuta unaovunja wa mita 3 au zaid unaingia gharama ya takriban laki 5.

Hapa ni lazima kuzingatia mahusiano ya vyumba, mfano kuna nyumba mlango wa jikoni upo pa kulia, na wa pa kulia upo sebuleni. Maana yake, mtu anaetaka kwenda jikon ni lazima apite sebuleni, sasa vuta picha una wageni na kuna Lajna yupo nje hana kiremba na anataka kwenda ndani akavae.... Mfano mwingine unabuni nyumba na gereji ya gari moja ndani kisha nyumba unaweka fence na mlinzi, mara nyingi hugeuzwa stoo tu huko mbeleni maana hainaga maana! Ukiwa na gari kali 2 ipi utaweka gereji na ipi utaweka kwenye tent nje, unaishia kuweka zote kwenye tent.

Yapo mengi sana ya kuzingatia.

3. Tumia wataalamu

Kishule shule tunafundishwa kuwa kwenye ujenzi kuna Client(Mteja), consultant(mshauri) na contractor(mjenzi). Client anamuajiri consultant amshauri na kumsaidia kusimamia ujenzi, afu pia anamuajiri contractor kujenga. Consultant anahakikisha client anafanyiwa kazi nzuri. Iyo ni kishule shule na ipo kwenye ile miradi mikubwa mikubwa. Kwenye miradi yetu ya kijumba cha vyumba 3 hatutumii hiyo, huku client anaajiri contractor kazi imeisha. HAPA SASA NDIPO TUNAPOKOSEA, tunapoamua kumruka consultant ndipo tunapofanya kosa. Wewe kama daktari, mhasibu, mwalimu, dereva n.k umeajiri mtu akujengee, ni nani anayehakikisha jengo lako linajengwa kwa kiwango kinachotakiwa? Ni nani anayehakikisha makosa wanayofanya mafundi yanasahihishwa? Ni nani atawafanya mafundi kuwa makini zaidi wakijua kuna mtaalam atakuja kukagua? Ni muhimu



sana uwe hata na rafiki injinia, fundi au hata mtu anayejua sana juu ya ujenzi ambaye utakua unampeleka site kwenye hatua nyeti e.g setting out, unampeleka site kukagua kazi zilizofanywa n.k atakuingiza gharama ya usafir labda na vihela kidogo lakin atakuokoa na kuingia gharama kubwa sana uko baadae.

Wote tunamkumbuka Mhandisi



Tahir Mirza, shughuli aliyokuwa anafanya pale Masjid salam wote tulikuwa tunaishuhudia na mwisho wa siku tunayaona matunda. Sasa yule alikuwa sehemu ya *Consultant* wetu wa ndani. Nilikuwa mafunzoni (field) chini yake, kwa hakika ubora wa kazi aliokuwa anauhimiza kikwetu kwetu unaweza kuupata kwenye ujenzi wa Ikulu au hoteli ya kifahari!!

4. Jua unachotaka

Kuna nyakati unapaswa kuamini mawazo yako na kufanya maamuzi ilimradi tu hayaathiri usalama wa jengo. Kwa watu wengi kujenga nyumba yako ni jambo linalobeba hisia kwamba «sasa najenga nyumba yangu» na kuna mambo mengi ungependa yawepo kwenye nyumba yako. Kwa sisi wataalam mfano mimi nipo kwenye tasnia kwa miaka 8 sasa, tunajenga kila siku na hatusisimuki tena kwamba tunajenga bali kila ujenzi kwetu ni kazi tu kama ilivyo kupiga mswaki, kuchana nywele na kuvaa viatu, ni kawaida ila kitu kinachotusisimua ni kumaliza kazi na kupata kazi nyingine, hivo mteja ni lazima uwe unajua unachokitaka vinginevyo mjenzi atakuwekea kilicho chepesi kwake ili amalize kazi.

Mwisho

Usikurupuke kwenye kujenga, utapoteza hela au unaweza usipate unachotaka. Fuata hatua, kuwa mjanja utajenga vizuri.

Tumia wataalamu, wameenda shule, wamesoma masomo magumu, wamekaa field, wamehitimu, wamefanya kazi miradi mbalimbali, wana uzoefu... Tusiwachukulie poa, tunawahitaji sana, sana.

Nawaombea wote kwa Allah tuweze kujenga nyumba zetu vizuri, Amin.

Abdul Latif Mosse
0718 - 55 00 20

Buriani Mwakitalima, Tutakukumbuka

Na **Yuusuf Mgeleka**
Kahama

Innalillahi waina ilaih raaji'un. Ilikuwa ni Jumanne tarehe 25.05.2021 majira ya adhuhuri, ghafla nasoma jumbe mbalimbali kwa mitandao ya kijamii (Whatsapp) zikielezea juu ya kifo cha mpendwa wetu Naib Amir Jamaat (Utawala) ndugu Issa Mwakitalima, Innalillahi waina ilaih raaji'un. Ni huzuni kubwa sana, simanzi kutanda.

Muungwana na mnyenyekevu ndugu yetu Issa Mwakitalima ametangulia mbele ya haki, hatunaye tena hapa juu ya dunia, ametangulia kwa Mola wetu. Namuomba sana Allah ampokee mtumishi wake huyu aliyejawa huruma na unyenyekevu mkubwa kwa sisi tuliomshuhudia, binafsi nitaelezea baadhi ya mambo machache sana ambayo nilibahatika kufanya nae kazi maalum za Jamaat huku yeye akiwa ndie msimamizi wangu mkuu.

Nakumbuka ilikuwa ni mwaka 2019 mapema asubuhi nikiwa nyumbani kwangu mjini Kahama, nikapokea simu ya Naib Amir Mwakitalima sahib. Nikaipokea simu yake hiyo na marehemu akaniambia "samahani sana kaka, hapa Dar es Salaam tumeandaa semina ya malezi ya wanandoa itakayofanyika Kitonga siku fulani ya Jumapili mwezi wa tatu au wanne (kama sijakosea). Akaniambia juu ya malengo ya semina hiyo kufuatia wimbi kubwa la changamoto za ndoa, akaniambia nimekupangia mada moja uiwasilishe siku hiyo." Hapo tayari nikaiona simu hiyo imekuwa ni nzito kwangu, nikamkubalia na akaniambia "kaka usiwe na wasiwasi, mimi nakuamini na najua kabisa unaweza kuwasilisha mada nitakayokupangia bila shida". Akazidi kuniambia, mie nawajua wanajamaat wengi, nimekuchagua wewe na nakuamini, hata kama upo mkoani ila nahitaji uje na utawasilisha mada maalum siku hiyo. Akanipa muda wa kujiandaa, na akaniambia mimi sina haja ya wewe kunitumia hotuba uliyoiandaa na niikague, **nakuamini kaka.** Kisha akaniambia mimi nakusubiri siku hiyo uwepo na uwasilishe mada niliyokupatia, nikaridhia na kumkubalia kisha nilisafiri mpaka Dar es Salaam ili niweze kutekeleza hotuba hiyo. Ikumbukwe kuwa sijawahi hata siku moja kutoa hotuba na kuwasilisha mada yoyote katika hadhira za Jamaat hususan Markaz, Dar es Salaam. Hiyo ikawa ni mara ya kwanza.

Basi siku moja kabla ya kuifikia Jumapili tarajiwa, nyakati za usiku Naib Amir Jamaat alinipigia simu kuniuliza iwapo nimeshafika Dar es Salaam tayari kwa semina kesho yake. Nikamjibu kuwa naam Alhamdulillah nimeshafika tayari Dar es Salaam, akaniuliza na je umeshajiandaa? Nikamjibu kuwa naam, nimejiandaa. Hapo akanishukuru sana na akasema hana khofu nami, hivyo kesho Jumapili saa nne tukutane Jalsa Gah pale Kitonga InshaAllah.



Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akimtambulisha Naib Amir Bw. Issa Mwakitalima kwa mgeni wa kikao cha kwanza katika Jalsa Salana 2017, Mh. January Makamba

Alhamdulillah siku hiyo muda ukafika wa kuanza semina, ghafla nimepangwa na wakufunzi magwiji wa kuhutubu na ikatangazwa kuwa mada ya kwanza itawasilishwa nami. Basi hapo nikasoma dua chache ili Allah anisaidie na niwasilishe vema mada husika. Nilianza khutba yangu nikiwa na hofu, waila nilijaaliwa kupata nguvu na kujiamini kwa kile ninachokiwasilisha, na nikawasilisha mada yangu mpaka mwisho.

Baada ya kuisha kwa semina, nakumbuka Naib Amir Jamaat alinifata na kunipongeza sana kwa maneno yafuatayo **Kaka nashukuru sana, umetoa** hotuba **nzuri sana na umenivisha nguo. Maana watu wengi walinifata na kunilalamikia kuwa inakuwaje unampa mada bwana Yuusuf Mgeleka na ukawaacha wakufunzi hodari wenye heshima zao kuwasilisha mada?"** Naib Amir sahib hapo akarudia, "yaani kaka umetoa majibu kwa wote walioniletea kejeli juu ya uwezo wako", mie niliwaambia kwa kuwajibu "mimi kama Kiongozi namuamini huyu bwana na muacheni, sitobadili msimamo". Haya yalikuwa ni maamuzi ya ujasiri sana aliyokuwa nayo Naib Amir sahib kwa kumuibua mtu kutoka mkoani, na akawaacha watu wengi maarufu wanajamaat wa jijini Dar kuhututubu. Itambulike kwamba hapa sikuomba nihutubie, na wala haijawahi hata siku moja kumuomba Allah kwamba siku moja nihutubu, ni kazi ngumu sana na ambayo huwa naikwepa mno. Lakini hapa tutaona ni kwa namna gani Allah alimjaalia karama pana sana ya kiuongozi Naib Amir Mwakitalima kufikia kuona na kuwamulika anaowaongoza na kuwaibua, kupitia semina hiyo binafsi nilipokea kongole nyingi sana kutoka kwa ndugu mbalimbali kwamba leo umetoa hotuba nzuri sana ambayo hatukuitegemea. Na kwamba hatukutegemea kama wewe unayo haiba ya kuhututubu na ukasikilizwa vema, nikamshukuru Allah kwa Alhamdulillah. Wapo ndugu wengine walionifata na waliomfata marehemu Naib Amir sahib na kumwambi kuwa, hivi kumbe wapo ndugu wazungumzaji wazuri hivi na tumewaacha, huyu bwana ingefaa hata kwenye Jalsa apewe mada na awasilishe. Na ikiwa haitoshi, Naib Amir sahib alinitumia mpaka ujumbe maalum wa simu kunishukuru tena, na kuniombea dua njema sana. Hakika tumeondokewa na kiumbe mnyenyekevu sana katika Jamaat ya Tanzania, namuomba Allah amrehemu Naib Amir Jamaat Issa Mwakitalima sahib, Aamin.

Jambo jingine ambalo nakumbuka vema na ambalo lilinifanya niwe karibu mno na Naib Amir sahib Issa Mwakitalima ni juu ya Jalsa Salana za Kitaifa. Kwa miaka 3 mfululizo nilifanya kazi nae nyeti sana, nitasimulia namna ambavyo niliwajibika nae.

Jalsa za mwaka 2017, 2018 na 2019 (nje ya majukumu mengine) mimi na Naib Amir Jamaat tulipewa jukumu maalum na Amir Jamaat juu ya wageni kutoka nje ya nchi. Kwa miaka hiyo mitatu mfululizo tulipokea wageni mbalimbali kutoka Kenya, Uganda, Pakistan, na nchi nyinginezo. Kama tujuavyo hatukuwa na maandalizi maalum na mazuri kwa ajili ya wageni wetu kutoka nje ya nchi, mara kadhaa nakumbuka sana kauli zake kwangu akiniongoza na kuniambia "Kaka, ujue hii jukumu ni letu mimi na wewe. Jukumu hili nakuachia wewe kwa asilimia 100 ulitekeleze, utakapokwama mahala popote basi uniambie". Hakika lilikuwa ni jukumu zito sana, na nililazimika kutoka Kahama mapema walau wiki moja kabla ili kuwahi kufika Kitonga na kuanza mipango yetu, wakati huo ikumbukwe kwamba mimi nilikuwa ndio msimamizi mkuu wa Maonyesho sambamba na jukumu hilo maalum. Ilinilazimu niwahi kufika Kitonga na kuweka mipangilio mizuri upande wa maonyesho, kisha siku moja kabla ya Jalsa nililazimika niwepo Markaz mjini kwa ajili ya kuanza kuwapokea wageni maalum kutoka nje ya nchi.

Naib Amir Mwakitalima akawa ananiambia, **"kaka, tuhakikishe tunawapokeaje wageni, wanalala wapi, wanakula nini, na kisha tuangalie namna ya kuwatembeza jijini mara baada ya Jalsa. Nikamwambia sawa Naib Amir nimekuelewa. Akaniambia tena kuwa, kaka ujue bajeti pia ni muhali hivyo tujipange sana tusipate aibu, tukipata aibu basi ni nchi ndio imepata aibu"**. Nikamwambi sawa na InshaAllah tutafaulu Naib Amir sahib.

Katika Jalsa ya mwaka 2017 tulipatwa na msiba wa Amir mstaafu mzee Ally Mosse, nakumbuka Naib Amir Jamaat hapa akaniambi "kaka, inabidi wageni wetu tuone wanaondokaje Kitonga na kuhudhuria maziko pale Wailes, naomba utasimamia chai yao na usafiri ili wafike makaburini. Mimi nitaamkia nyumbani Tuangoma kuandaa chakula chao cha mchana kisha niwahi kwenye matayarisho na maandalizi ya mazishi ya Amir sahib mstaafu, utakuja na wageni wote na tutaondokea Wailes mara baada ya kuzika InshaAllah". Nikamjibu sawa Naib Amir sahib na usiwe na wasiwasi wowote, wageni wote watafika bila shida

Endelea uk 10

Bustani ya Washairi

KWELI HUU NI MSIBA

1. Kweli huu ni msiba, hii ni inna lilaahi
Isa niliyemshiba, kafariki asubuhi
Pengo lisilo wa kuziba, faraja ni tasbihi
Huu ni inna lilaahi, kweli huu ni msiba

2. Chungu hii tajiriba, moyo imenijeruhi
Na chakula nikashiba, zama nimetanabahi
Si msiba ni dhoruba, ya rabbana, ya ilahi
Hii ni inna lilaahi, kweli huu ni msiba

3. Mwakitalema habiba, hukuwahi nikirihi
Mchamungu wa haiba, mpole mwenye stahi
Mola akupe maaba, huko peponi uwahi
Hii ni inna lilaahi, kweli huu ni msiba

4. Pole amiri sahiba, poleni nsarulahi
Kumfanya ni naiba, ilikuwa ni sahihi
Machoziye si ya haba, nidhamu kiikebehi
Hii ni inna lilaahi, kwewli huu ni msiba

5. Ninakuomba ya rabba, familia isitahi
Kuondokewa na baba, wasibaki fukarahi
Na mzidi kwenye toba, nawasihi nawasihi
Huu ni msiba, hii ni inna lilaahi

Amiri Kaluta
Dar es salaam

ISSA UMETANGULIA

Kwa Mola Mola wetu Rabana, kinyonge nakimbilia.
Namuomba Sub-hana, subira kunikidhia.
Kilio kimenibana, nashindwa kujizuia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Tumebaki na simanzi, sote tunakulilia.
Twatiririsha machozi, na macho yamevilia.
Kwa kweli hatujiwezi, nyoyo zatuzizimia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Bwana Isa Anangisye, wewe nilijivunia.
Wema wako kwangu mie, ninapo ukumbukia.
Acha kwa kwikwi nilie, huzuni yanizidia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Sahibu wangu kipenzi, tuzo nakutunukia.
Ulikuwa mwanagenzi, kundini ulipongia.
Kisha ukapanda ngazi, sote ukatuzidia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Hata ukawa Naibu, wa Amiri Tanzania.
Kiongozi mahababu, muadilifu sawia.
Mwenye mema matulubu, ya dini kutumikia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Hakikuja kwa bahati, cheo ulichofikia.
Ulijitoa kwa dhati, kwenye njia ya Jalia.
Kwa sadaka ya wakati, mali na nafusi pia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Ulikuwa mtu mwema, kwenye hii jumuiya.
Kidete ukasimama, dini kuipigania.
Na hukuenda mrama, kwa lawama kuhofia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Upande wa mahubiri, huna wa kufanania.
Hukuhofu maayari, neno kuwafikishia.
Na haja zilipojiri, nyingi uligharamia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Kwa kujitolea mali, katu haukusinzia.
Vyako ulivisabili, vikawa vya jumuiya.
Na hata ulijidhili, dini ukasaidia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Fakiri na masikini, Isa hukuwakimbia.
Uliwapa masikani, na ukawahudumia.
Na kwa hili Rahamani, mema takuzidishia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Ulikuwa na bashasha, hukujua kuchukia,
Hakunaye wa kubisha, hili ninohadithia.
Hakika yako maisha, ni somo lilotimia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Hata kwenye timbwiliko, la kutafuta dunia.
Ulitenga muda wako, Mola kumhimidia.
Hata kwa ahali zako, sala ulihimizia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Niwape pole vizuka, yatima ulotwachia.
Nawaombea Rabuka, wasiache yake njia.
Awaondoe mashaka, Awakinge na udhia.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Tutakumbuka daima, maombi kukufanyia.
Na tutatimiza dhima, ulizozikusudia.
Nenda kalale salama, kwenye pepo ya Karima.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Kwa huyo Mwenyezi Mungu, uliyemuitikia.
Tutakutana kidugu, zama zitapowadia.
Kwani sote ni wa Mungu, na kwake tutarejea.
Issa umetangulia, tumebaki na simanzi.

Abdullah H. Mbanga (Kungwi)
kungwi504@gmail.com

KIZAZI_TEULE

Ni kizazi teule, Kijukuu cha sahaba
Kilo vikwa usukule, Kwacha ya dini mahaba
Kilo sahau ya kale, Kumbu ni visa nasaba
Siye warithi wa Yule, Masihi muahidiwa

Neema nyingi hulevya, Hula nguvu ya maombi
Rohoni Uja huavya, Kumfanya mja zombi
Salani huanza chovya, ndipo hugeuka pimbi
Zisitulevye laghui, Na anasa za dunia

Shunda Mshudia wana
Daluni, Tanga

JIUNGENI NAMI

Mie jua la Baraka, Sayari nizungukeni
Na kwenu sina Mipaka, Mpatapo nizuruni
Na msipo bahatika, Kwa barua sabahini
Kwa waso elimika, Niwekeni sujudani
Ni sauti iitayo, Upande wa Ukhalifa

Shunda Mshudia wana
Daluni, Tanga

DAWA NENDA KWA MOLAO

Mambo yakikulemea, usipoteze wakati
Kutwa kiguu na njia, kwa wale wasaka noti
Si waganga nakwambia, haja yao sharubati
Dawa nenda kwa Molao, upate tiba kamili

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani

TUNZA HESHIMA YAKO

Itunze heshima yako, kuacha jambo fulani,
Usije kuwa kituko, sababu kitu fulani,
Anguka kwa mola wako, utapata auheni,
Muombe sana manani, Akuze yako imani.

Muombe sana manani, akuze yako imani,
Aepushe mitihani, usiwe majaribuni,
Jambo baya libaini, usipoteze imani,
Itunze heshima yako, Kuacha jambo fulani.

Kalamu naweka chini, kauli yangu natoa,
Naomba uwe makini, katika kila hatua,
Bado upo safarini, mzigo hujautua,
Itunze heshima yako, Kuacha jambo fulani.

Saliana Ramadhani Higiro

VILIJE MNANG'ATUKA

Kwa jina lake ilahi, ninaanza kuandika
aso na wake wajihi, si tunao ukumbuka
mletaji Asubuhi, bada Kiza kuondoka
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Salaamuna Alayhi, zimuwie msifika
aliye rasulullahi, kipenzi chake Rabuka
Waa'laa asw-habihi, jimaina kadhalika
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Nahii si tanbihi, ni hoja ya msumbuka
taraa nisiwe sahihi, kunradhi natamka
sijui kiufasahi, sababu ya kuondoka
Enyi Jeshi La Masihi, vilije mnaondoka?

Kutaraghika sahihi, bumbuwazi lanishika
waongoza kusabihi, ghafla mnatimka
zama hizi majeruhi, nguvu kazi kuyeyuka
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnaondoka?

Enyi Jeshi la Masihi, vilijemnang'atuka
tatizo ni maslahi, ama lipi la hakika
pa kuku chini kuvihi, Ettamaa-Mewashika
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Lipi linawakarihi, hadi mnatawanyika
tubulunge kifasihi, kwa tungo zinazoshika
ikifaa tuwasihi, huenda wakaitika
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Twapataje Uswalihi, Wasomi mnatimka
twasomaje kisahihi, Kurani so majaka
mkumbushao nanihii, michango mnatoweka
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Jumuiya ya Masihi, Mola ameisimika
jioni kwa Asubuhi, inazidi kupanuka
msiache kazi hii, ya wito yenye Baraka
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Vilinge vinawasihi, na Ghumma imewashika
alowakwaza ni yuhi, yu Mtu atafutika
Maji kupwa zamahii, Taqwa imetoweka
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Mwenye jambo fuadihi, atakwa kulianika
Mafuriko yamebihi, Wimbi la wanong'atuka
Kus Kas Tanga bahi, Walimu watuponyoka
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Tupigeni Tasbihi, kumsabihi Rabuka
Sala isitukirihi, Maghfira kuyataka
Mahabbuna a'layhi, atupende kadhalika
Enyi Jeshi la Masihi, vilije mnang'atuka?

Ibn Habeeb
Dar es salaam, Tanzania

MAISHA NI MZUNGUKO

Maisha ni mzunguko, ulipo kweko tatoka, Wengine walikokweko, wewe huko utafika, Kila siku badiliko, mwisho mauti tafika, Tumia nafasi uko, sijutie ikitoka.

Masihi Omary Stambuli (Kisagwa)

YALIYOPITA SI NDWELE

Bado nafasi unayo, sikae bali SIMAMA
Makovu katika moyo, ni bado yanakuuma
Shime yasahau hayo, yanachafua mtima
Yaliyopita si ndwele, ugange yanayokuja

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani

Mti wa matufaa



Hapo zamani, palikuwa na mti mkubwa wa matufaa. Mvulana mmoja alipenda kwenda na kucheza nao kila siku. Alipanda juu kabisa, alikula matufaa. Alilala kwenye kivuli chake. Aliupenda mti na mti ulipenda kucheza naye.

Muda ukasonga. Mvulana sasa akawa kijana na hakucheza kule mtini tena. Siku moja, kijana alirudi kwenye mti na akagundua kuwa una huzuni.

" N j o o ucheze nami" mti ulionekana kumuomba kijana. "Mimi sio mtoto tena, sichezi kwenye miti," kijana alijibu. "Nataka vikorokoro vya kisasa vya kuchezea. Nahitaji pesa kuvinunua."



"Pole, lakini sina pesa, ila waweza chuma matufaa yangu yote na kuyauza. Ndipo utapata pesa." Kijana alifurahi sana. Alichuma matufaa yote mtini na akaondoka akiwa na bashasha. Kijana hakurudi tena baada ya kuchuma matufaa. Mti ulihuzunika tena.

Siku moja, miaka mingi baadaye, kijana aliyekuwa sasa mwanaume akarudi na mti ukafurahika sana! "Njoo ucheze nami," mti ulionekana kusema. "Sina muda wa kucheza. Inabidi nifanye kazi kwa ajili ya mke wangu na watoto. Tunahitaji nyumba ya kujistiri. Unaweza nisaidia?" mwanaume alijibu.

"Samahani, sina nyumba yoyote. Lakini unaweza kukata matawi yangu kujengea nyumba yako."

Basi mwanaume akakata matawi yote kwa furaha na kuondoka akitabasamu. Mti ulifurahi kumuona tena lakini mwanaume hakurudi tena kwa miaka na miaka. M t i ulikuwa mpweke tena na ukakasirishwa.



Siku moja ya kiangazi, mwanaume alirudi na mti ukafurahi. "Njoo ucheze nami," mti ulisema. "Nakaribia miaka hamsini. Nataka nipige tanga ili niburudike kipindi cha likizo. Unaweza kunipa jahazi?" aliuliza mwanaume.

"Tumia kiwiliwili changu kujengea jahazi lako. Utaweza kupiga tanga mbaali na ukaburudika," mti ulionekana kujibu.
Basi mwanaume akaukata mwili wa mti kwa furaha kutengenezea jahazi. Akaenda kupiga tanga na hakurudi kwa kitambo kirefu.

Hatimaye, mwanaume alirejea baada ya miaka mingi. "Samahani kijana wangu. Lakini sina chochote kwa ajili yako tena. Sina matufaa," mti ulionekana kusema.

"Hakuna tatizo, sina meno tena ya kung'atia," mwanaume alijibu

"Sina mwili wa kunipanda tena," mti ulionekana kujibu.

"Nimezeeka sana kwa hilo sasa," mwanaume alijibu.

"Kweli siwezi kukupa chochote kijana wangu. Kitu pekee nilichobakia nacho ni mizizi yangu inayojifia," mti ulionekana kusema na machozi.

"Sihitaji mengi sasa, sehemu tu ya kujipumzishia. Nimechoka baada ya miaka yote hii," mwanaume alinena.

"Vyema! Mizizi inayojizeekea ndio sehemu nzuri ya kuegema na kupumzika, njoo ukae nami kitako upumzike," mti ulionekana kunong'ona kimoyomoyo.



Mwanaume akakaa kwenye nyasi akiegemeza mwili wake dhaifu kwenye kisiki. Mti ulifarijika sana hata ukaonekana ukitabasamu kwa machozi...

. . . . . .

Hadithi hii inatufundisha nini?

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 25 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

R	M	M	S	N	G	R	X	D		J	T	L	T	A	H	R	I	K	
T	K	X	A	B	M	V	H	A	Q	N	M	S	I	K	I	T	I		M
Z	F	N	N	D	L	W	B	G		M	A	K	A	L	A		M	K	A
K	Z	V	D	H	P	I	A	A	W	M	Z	K	M	N	J	D	L	J	U
M	M	H	A	X	T	D	N	L	L	T	A	H	K	B	N	Q	N	T	U
T	Y	Y		A	Y	A	M	F	I	Y	T	S	K	F	R		X	Z	D
C	A	Q	K	G	L	Z	Z	L	T	M		N	I	M	A	I	T	I	
Q	S	P	M	U	V	K	X	A	A	A	U		P	H	G	R	G	N	J
X	S	M	A	A	R	B	Y	B	H	H	U		S	P	I	M	Z	K	K
N	A	M	A	J	Z	Y	A	S	R	M	M	A	N		J		M	B	Q
P	R	Q	K	S	I	I	I	R	E	L	R	A	I	L	R	M	W	U	B
W	N	N	L	S	H	M	S	H	A	B	T	N	D	M	W	M	F	K	M
N	A	M	A	C	I	A	E	H	A	B	A	M	V	I	Z	Z	J	H	U
P	L	W	C	S	Z	R	I	K	I	I	A	P	R	X	Y	Y	A	A	O
R		D	A	N	A	Y	D	R	R		Z	R	R	C	M	Y	M	R	N
P	P	R	D	M	N	D	L	U	I	L	L	P	A	R	Z	G	A	I	G
C	R	Z	Z	P	N	T	B	Q	T		Q	T	Z		M	H	A		O
K	F	K	T	M	H	G	K	R	C	N	L	C	N	H	N	T	T	G	Z
T	K	D	F	A	L	S	A	F	A		W	R	M	B	Y	G		L	O
M	W	M	W	G	N	M	T	U	T	A	M	B	U	Z	I		Y	M	

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Biskuti za Jam

Na **Mtandao**



Mahitaji



1. Unga vikombe 2½
2. Sukari ¾ kikombe
3. Samli kikombe 1
4. Mayai 2
5. Baking powder Vijiko 2 vya chai
6. Vanilla Kijiko 1½ cha chai
7. Ganda 1 la chungwa

Jinsi ya kutayarisha na kupika

1. Tia kwenye machine ya kusagia (blender) mayai, sukari, vanilla, samli na maganda ya chungwa, saga vizuri.
2. Tia unga kwenye bakuli pamoja na baking powder, mimina vitu ulivyosaga kwenye bakuli, changanya.
3. Punguza unga uliochanganya kidogo weka pembeni.
4. Unga uliobakia tia kwenya tray ya kuchomeya, utandaze vizuri, tia jam juu yake.
5. Chukua la kukwaruzia carrot (grater) ukwaruze unga uliuopunguza juu ya jam.
6. Choma kwa muda dakika 20 moto wa 180 C.
7. Acha ipowe kidogo, zikate vipande vya mraba (square) Tayari kwa kula.

N.B: Jiko la mkaa si zuri sana kwa kupata matokeo bora

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA AS

Kudhihiri kwa Mwenyezi Mungu

Naam, Mweza wa yote na Mwenye nguvu ni yule Mungu Ambaye Waumini Wake hawatahasirika kamwe; wale wamjiao kwa mapenzi na uaminifu. Adui hujigamba kwamba atawaangamiza wote kwa ushetani wake na mwenye nia mbaya huapa kwamba atawamaliza. Wapumbavu ninyi, Asema Mwenyezi Mungu, je, mtajasiri kupigana nami? Na kumdhalilisha yule aliye mpenzi wangu? Kwa hakika, lolote haliwezi kuikumba dunia hii ila liwe limekadiriwa hivyo huko mbinguni, wala hakuna mkono wa kidunia uwezao kufikisha dhoruba zake nje ya eneo ulilopimiwa huko mbinguni. Hivyo basi, wenye kula njama za uovu na ukatili ni wapumbavu mno ambao katika harakati za mipango yao miovu ya aibu, hawamkubali Yule Dhati Mkuu Ambaye hata jani haliruhusiwi kudondoka bila ya amri Yake. Kwa hivyo, wao huibuka na kushindwa na shabaha zao kutotimia; wala njama zao haziwadhuru wale walioongoka; kinyume chake ishara za Mungu huenea zaidi na fahamu za watu juu ya kudra ya Mwenyezi Mungu huongezeka. Yule Mungu Mweza, Mwenye nguvu, Asiyeonekana kwa macho, Hujidhihirisha kwa hakika kupitia kudra Zake za ajabu.

(Roohani Khazain Jal. 13: uk. 19: Kitab-ul-bariyya, Muqaddama uk. 1)

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Kujitakasa ni katika njia ya radhi ya Allah

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

(ٱلَّذِى يُؤۡتِى مَالَهُۥ يَتَزَكَّىٰ)

Ambaye hutoa mali yake kujitakasa. Surah Al-Layl 92:19

UTAKASO ni njia ya kukifanya chema 2:130. Mwanadamu amezungukwa na Mali, vitu na watu. Maisha yake yote huhitajika kuwa Mema na ya Uchamungu mpaka vitu anavyotumia na vilivyomzunguka. Wakati fulani mwanadamu hufanya Jitihada za kuwa mwema kwa kutenda matendo mazuri na Mema. Jitihada hizo huwa hazitoshi kumfanya Mwema aliyekamilika ikiwa Mali na vitu anavyotumia na vinavyomzunguka vikiwa vimebeba vinasaba vya Uovu. Hii hutokana na Mali na vitu halali kukaa muda mrefu basi muda unavyopita Uhalali wa vitu hivyo hukosekana na kugeuka kuwa viovu na kuvitumia kwake Mwanadamu huanza Kumeza Uovu. Au Kukaa na Kutumia na vitu viovu huku akiwa Mwema basi hutafuna wema wake.

Mfano Mali halali iliyokaa Mwaka mzima mali hiyo sio halali tena kuitumia kabla ya kutoa Zaka. Kipato kilicho chumwa sio halali kabla ya Kujitolea Chanda ukiitumia bila kutoa basi utakuwa unakula Uovu na hatima yake kuwa Muovu. Tunatakiwa kujitolea Sadaka kwa ajili ya Ustawi wa watumishi wa Dini na Masikini na Ndugu na Wasafiri na Wenye matatizo kwa kila kipato chako halali na usipofanya hivyo utakuwa unauwa Moyo wako na Huruma kutoweka na hatima yake ni Uovu. Nafsi inapaswa kuendelea kusikia na kupata mawaidha mema kila wakati na kwa uchache kwa wiki mara moja ikaandaliwa kama siku ya Ijumaa na Mtu asipopata mawaidha kwa muda mrefu angalau wiki tatu nafsi yake inakufa.

Ili Mwanadamu Adumu kwenye Wema yampasa kwanza vitu vinavyomzunguka vyote na anvyotumia Vitakasike na ndipo aweze kuishi na Kukaa kwa wema. Wema wetu unaweza kuwa unaenda ukipungua na kupotea kwakuwa tunaishi na kukaa na vitu visivyo takasika. Na maana dhahiri ya Utakaso ni Mali. Mali inanunua kila kitu chako. Haupo Wema au Ibada yeyote ila Imeambatanishwa na Utakaso yaani Kujitolea Mali na Nafsi. Sala bila Utakaso haistawi wala Matendo Mema bila Utakaso ni Jitihada zinazopotea kwa Urahisi. Njia ya Utakaso ni katika Radhi ya Allah na Radhi ya Allah ni mlango wa Ufunguo wa kila kitu akiitajio Mwanadamu pamoja na Riziki.

.....hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaotubu na wanaojitakasa. Surah 2:223

Mola wetu, Ututimizie nuru yetu, na Utughofirie; hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. Amin

TANGAZO LA IJTIMAA YA MAJLIS KHUDDAMUL AHMADIYYA TANZANIA

Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inapenda kuwataarifu Khuddam na Atafal wote nchini kuwa Ijtimaa yao itakuwa tarehe 18-20 Juni 2021, Kitonga, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.

In-Shaa-Allah.

Khuddam na Atfal wote wanaombwa kuendelea na maandalizi ya Ijtimaa hii na kuichangia pia sawa na matakwa ya katiba.

Usipange kukosa!

Limetolewa na Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania

MATUKIO KATIKA PICHA



Mkuu wa Jamia Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Abid Butt akisalimiana na Mkuu wa Wilaya katika futari iliyoandaliwa naye.



Picha ya pamoja ya wanajamaat wa Malawi baada ya sala ya Idi-el-Fitr



Mkuu wa Jamia Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Abid Butt akiongoza sala ya Idi-el-Fitr katika viwanja vya chuo hicho



Atfal na Nasrat wa tawi la Nyanhokolwa, Simiyu wakifurahia zawadi katika sikukuu ya Idi-el-Fitri



Maadhimisho ya Siku ya Ukhalifa yaliyofanywa na Chuo cha Jamia Ahmadiyya kilichopo Morogoro



Sheikh wa Mkoa wa Dodoma akikabidhi zawadi ya Idi kwa viongozi wa gereza la Dodoma kwa ajili ya wafungwa



Khuddam wa Mtwara Mjini wakijitolea damu kusherehekea sikukuu ya Idi-el-Fitr



Mashindano ya Qur'an Hifdh na Tilawat katika mwezi wa Ramadhan kwa Khuddam na Atfal wa Mtwara na Masasi

Buriani Mwakitalima, Tutakukumbuka

Kutoka uk. 5

kwenye mazishi, na mipangilio yote itaenda sawa usiwe na wasi. Akasema, "sawa nashukuru sana kaka na Mungu akujaalie sana". Nikamjibu Aamin. Ikumbukwe katika Jalsa hii ya mwaka 2017 tulitembelewa na wageni kutoka Uganda takriban 9 ambao ni wanaume na Lajna mmoja, hivyo ilikuwa ni jukumu zito kwetu kumudu kwani baadhi ya wageni hao walifika kwa ndege, wengine kwa bus. Naib Amir Jamaat aliniagiza "kaka naomba usimamie kuwasili kwao na kuondoka kwao, usimamie wewe mwenyewe kwa mkono wako". Nami nilitekeleza maagizo yake hayo, Alhamdulillah.

Katika miaka hiyo yote mitatu tukiwajibika kuitumikia Jamaat kwenye Jalsa Salana, Naib Amir Mwakitalima licha ya nafasi yake kubwa anayoituikia lakini daima alikuwa akitumia lakabu kuniita pale anaponiagia kwa jina la **"kaka"**, ukizingatia hata umri alikuwa amenizidi. Alidumu sana kuniita kaka, na kisha tunashauriana mambo kadha wa kadha. Hata kama itokeapo baadhi ya mambo kwenda mrama, lakini alikuwa akikaa kimya sana na kuniambi, sasa kaka hapa tufanyeje maana kila kitu tayari kimeharibika. Huku akiniambia "kaka mimi nakusikiliza tunafanyaje", kwa nyakati kama hizo daima nilikuwa nikimtuliza na kumwambia Naib Amir sahib naomba hilo niachie nipambane nalo na nitakupatia mrejesho InshaAllah. Yeye akinijibu "sawa kaka, nakutegemea". Hayo daima ndio yalikuwa hali ya maisha ya utendaji wake wa kazi kwa nyakati fupi ambazo nilidumu kuwa nae, na nyakati ambazo zilidumu kwa kutingwa mno shauri ya unyeti wa Jalsa ya Kitaifa.

Nakumbuka mwaka juzi pia wakati wa kuadhimisha Jalsa Salana ya miaka 50, hapa tulizidiwa zaidi kwa kuwajibika. Maana hapa tulikuwa na wageni wengi kutoka mataifa mengi zaidi, kama kawaida yake wiki moja kabla ya Jalsa akawasiliana nami kuw "kaka vipi umeshafika mjini?" nikamjibu. Basi hapo akaniambia inabidi tuje tukae maana tumekabidhiwa tena jukumu kubwa na zito zaidi mwaka huu, uje mapema ili tuangalie namna ya kuwapokea wageni wan je ya nchi, malazi yao nachakula chao. Maana mie hapa naumiza sana kichwa kaka. Basi, haraka haraka nikafunga safari kutoka Kahama kuja Dar ili tuanze maandalizi hayo na Naib Amir Mwakitalima sahib. Tukakutana na kupanga yote, na hapo tukaanza majukumu yetu. Ilikuwa ni kazi inayohitaji umakini mkubwa sana, na tulifaulu kwa kudra zake Allah. Nyakati zote Naib Amir alikuwa akinisisitiza kuwa "kaka ujue sisi ndio tumeibeba nchi hivi sasa, doa lolote litakalojiri kutokana na Jalsa Salana yetu kwa wageni waliotoka nje ya nchi basi ndio doa letu. Nakuomba kaka tuache majukumu yetu mengine yote na tujikite kwenye hili tu, najua hatutapumzika ila Allah ndie atatulipa au sio kaka, nikamjibu naam ni kweli Naib Amir sahib". Leo ameondoka, ni huzuni kubwa sana.

Naib Amir Mwakitalima ametangulia mbele za haki, ameniachia uzoefu mkubwa na mafundisho ya kuwahudumia wageni kutoka nje ya nchi. Na amenifundisha namna ya kutatua changamoto za wageni, na kuwasikiliza. Ameniachia alama njema ya kutambua ni namna gani ya kuwakarimu wageni kutoka nje, na kuhakikisha kila aina ya mahitajio yao basi tujitahidi kuyatimiza tena iwe mchana au usiku. Allah akupokee Naib Amir Mwakitalima.

Nipo mbali ndugu yangu Naib Amir Mwakitalima katika kukusindikiza safari ya hitimisho lako hapa duniani, waila dua zangu njema zipo nawe na Allah akujaalie makazi mema peponi, Aamin.

Namuomba Allah akusamehe madhambi yako yote hapa duniani, Aamin. Namuomba Allah akuimarishie familia zako na aviimarishe vizazi vyako vyote katika Islam Ahmadiyya na daima wafungamane na kamba ya Imam wa zama hizi, Aamin. Ewe Allah Mtukufu, tujaalie nasi tuwe ni wenye matendo mema na utujaalie tuwe na mwisho mwema hapa duniani, Aamin.

Hasara na madhara ya kutofanya mazoezi

Na **Ismail Abdul Nasibu**
Muhtamim Sihat-e-Jisman, M.K.A.T.

Kutofanyara mazoezi kuna hasara na madhara mengi. Baadhi yake ni:

1. Mwili huwa mzito, hukosa kuwa imara na huwa sio uliojiandaa kukabiliana na dharura

2. Kinga ya mwili hushindwa kuwa imara zaidi na utapata hata magonjwa na maambukizi madogo madogo

3. Uzito wa mwili kuwa mkubwa (obesity) na hatari kwa afya yako



4. Mwili unakuwa katika hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukizwa kama vile kisukari, presha, uzito mkubwa uliopitiliza (obesity), msongo na magonjwa ya moyo na mfumo wa damu

5. Kuwa na manyama uzembe, kitambi kwa akina baba na tumbo kubwa kwa akina mama

6. Mwili haujengeki vizuri na mtu huweza kukosa umbo zuri



7. Kuwa na mrundikano wa mafuta mwilini na kwenye mishipa ya damu – HATARI SANA!

USHAURI

Mazoezi huboresha afya, huzuia magonjwa.

Fanya mazoezi ili uweze kuishi muda mrefu. Sio lazima ufanye mazoezi magumu, ya gharama au mbali na ulipo – Anza na yale utakayoyamudu kwa urahisi.



Unaweza ukaamua kutembea au kukimbia umbali fulani kila siku, ruka kamba, nyanyua vitu vizito nk kulingana na nafasi yako.

Boresha maisha yako. Refusha maisha yako. Fanya mazoezi!...



Kwa nini *Biblia Ni Jibu* Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Na **Juma Iddy Abeid,** Kigoma

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

HOJA YA KUMBWA KWA ISSA

Mwandishi akiendelea ana sema Issa ndani ya Quran kumbwa kama ilivyo umbwaji wa Adam. 3:60 Bila shaka hali ya Issa kwa Mwenyezi Mungu ni kama hali ya Adam aliniumba kwa udongo kisha akamwambia kuwa basi akawa Akifafanua alivyo elewa Muandishi wa Biblia ni jibu anasema. Hivyo kwa mujibu wa aya hii Issa aliumbwa kama alivyoumbwa Adam alivyo tenda dhambi ndivyo na Issa alivyo mwisho wa kunukuu

Kwa hali hiyo inaonesha jinsi gani Mwandishi alivyo kuwa amaelewa Quran Na hilo sio ajabu kwani Mwenyezi Mungu Anasema katika Sura 17:46-47; Na unapo soma Quran tunatia baina yako na baina ya wale wasio amini Akhera pazia ilivyo sitiriwa.

Natumetia vifuniko miyoni mwa isije wakaifahamu na katika masikio yao mna uzito na unapomtaja mola wako wa pekee katika kurani basi wao hugeuza migongo yao kwa chuki huo ndio uhalisia.

Kwani aya inaonesha jinsi Issa alivyo patikani kwa kutumia neno la quni faya quni yani kama vile Adam alivyo kuwa kwa Mwenyezi Mungu alivyo sema kuwa akawa nafs hai ndivyo na Yesu alivyo patikana pwani nay eye aliumbwa kuwa tumboni akawa tumboni mwa mama yake Mariyam Ajabu eti mwandishi haelewi hapo ni kuwepo ni kwamba Mwenyezi Mungu alichokusuda hapo ni kuwepo kwao yaani wote wawili ni kauli moja tu ili tumika kuwa kisha wakawa.

Yaani Adam hakuwa na wazazi yani hakuwa na baba wala mama hivyo uwepo wakea ulitokana na neno la kuwa akawa katika mavumbi pia Issa hakuwa na baba, Na baba ndie huweka mimba kwa mwanamke. Hivyo kwakuwa Mariamu hakumjua mtu mume na yeye mimba ilipatikana kwa neno la kuwa ikawa mimba. huo ndio mfanano wa Issa na Adam, na si vinginevyo.

AKAJA NA HOJA YA NENO

Hapo mwanzo kulikuweko neno naye neno alikuweko kwa Mungu naye neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuweko kwa Mungu vyote vilifanyika kwa huyo wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika YOHANA 1;1-4 Kisha akaunga mwandishi na Yohana 17;5 na sasa baba unitukuze mimi pmoja nawe kwa utukufu ule nilikuwa nao pamoja nawe kawa ya ulimwengu kuwako.

Atasema Maandiko hayo yanathibitisha kuwa Yesu hakuumbwa bali ndie aliyeumba kila kitu. akasema hata huyo Issa wanae sema waislam ndani Ya Qurani aliubwa na huyo huyo Yesu kristo. hivyo kwa hoja ya uumbaji Issa na Yesu watu wawili tofauti. Hapo msomaji ndipo unatakiwa kuona jinsi muandishi wa *Biblia ni Jibu* anavyo tapatapa na alivyo muelewa na maandiko ukweli Yesu sio neno ila alitokana na neno, Neno lilitoka kinywani mwa Mungu lakuwa mimba ikawa tumboni mwa mama yake .na tamko hilo ndilo Mungu mwenyewe . Nasema hivyo kwa sababu vifungu hivyo havina tofauti na kitabu cha Mwanzo; 1:1 Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi Mwanzo 1:3; Mungu akasema iwe nuru ikawa nuru. Ina maana Mungu aliposema neno Nuru ikawa nuru mwanzo 1:6 Mungu akasema na liwe anga katikati ya maji Mwanzo 1:9 Mungu akasema maji yaliyo chini ya mbingu nay a kusanyika mahali pamoja Mwanzo 1:16- Mungu akasema Mwanzo 1:20 Mungu akasema Mwanzo 1:26 Mungu akasema.

Kwa vifungu hivyo kusema Yesu ndie neno muumbaji unakuwa umetumia akili gani? au akili ya rohoni? je Mungu kabla hajatamka vilikuwepo je si vyote vilifanyika kwa kutamka na Mungu? Je sura 19:20-23 (malaika) akasema hakikamimi ni mjumbe wa Mola wako ili nikupe mwana mtakatifu.Mariam akasema Nina wezaje kupata mototo hali hajanigusa mwanaume yeyote wala mimi si asherati? (Malaika) akasema ni kama hivyo: Mola wakoamesema haya ni rahisi kwangu na ili tumfanye Ishara kwa wanadam na rehema itokayo kwetu,

Basi (Mariam) akabeba mimba akaondoka nae mpaka mahali pa mbali huo ndio upatakanaji Issa kwa Mariam ni kwa neno tu.

Pia biblia inasemaje? Luka 1-31 tazama utachekwa mimba na kuzaa motto mwanaume na jina lake utamwita Yesu. LUKA 1:34- Mariam akamwambia malaika itakuwaje Neno hili? Maana sijui mume. kwa vifungu hivyo vya Qurani na biblia Issa ndio Yesu na Mungu ndie muumbaji kua neno sio Yesu

YOHANA 17:5 ni Maombi tu ya yesu kwa Mungu ambayo aina maana ya yeye kuwepo ila inaonesha anamuambia Mwenyezi Mungu alivyo panga toka Mwanzo wa mipango yake ya uumbaji kwani sisi sote hakuna aliye toroka kuja humu duniani au alie wahi au kuchelewa ila Mwenyezi Mungu anatuleta duniani kwa kutimiza mpango yake yatoka azali

UTABIRI

Hoja ya utabiri anasema hatuoni andiko lolote linalo mzungumzia utabiri Issa :Hivyo Issa hakutabiriwa Yesu ndani ya Biblia kuna tabiri 63 za manabii wakitabiri habari ya Yesu halafu akazitaja . Halafu akachekesha eti kwa kuwa Quran haikutabiri basi Issa Sio Yesu.

Kanuni ya utabiri huja kabla ya tukio Mwandishi angejiuliza kanuni hiyo alafu akajua Agano lakale na Qurani ni jawabu lakwanza ingetosha basi sie Isa. Hivyo ni vichekesho bora hata utabiri ungepishana ingekuwa hoja Qurani haiwezi kumtabiri mtu yaliyo mkuta. Ila kusimuliwa tu mfano na mwandishi mwenzangu wa Biblia ni jibu hatuwezi kumtabiri Mwalimu Nyerere ila tunacho weza ni kumsimulia tu. Hivyo hapo mwandishi alikosa hoja.

AKAJA KATIKA NASABA

Itaendelea toleo lijalo

Kukabiliana na Mateso na Ukandamizaji kwa Maombi na Huruma

Kutoka uk.12

kutambuasawasawa walikuwa wanafanya nini na kwa sababu gani. Hata siku moja nilimwona mtu mmoja akimsukuma kwa sababu ya uadui.

Kuhusu mambo haya Allah alikwisha mpa wahyi Masihi Aliyeahidiwa[as] katika sura ya shairi la kiajemi hivi:

اے دل! تو نیز خاطر ایناں نگاہ دار
کاخر کنند دعوئ حبِّ پیمبرم

Ewe moyo wangu wewe fumba macho yako kwani watu hawa wanakufanyia upinzani na uadui kwa sababu wanampenda Mtume[saw]. Yaani hawa wanakuchukia wewe kwa dhana kuwa wewe ni adui wa Mtume[saw]. Kwa hiyo haya ni kwa sababu ya mapenzi waliyokuwa nayo kwa Mtume[saw], kwa hiyo usihuzunike.

Khalifa mtukufu[atba] akaongeza kusema kuwa kwa hiyo sisi tunapokabiliana na upinzani na uadui kutoka kwa ndugu zetu Waislam kwa kashfa zao na matusi yao kwetu tunatakiwa kuwaombea dua na msamaha wa makosa yao badala ya kuchukia na kukasirika, na inatakiwa sisi tuwaelimishe hakika ya Masihi Aliyeahidiwa[as] na Jumuiya yake.

Mwisho wa siku ni miongoni mwa hawa hawa watapatikana watu watakaomwamini na kumfuata Masihi Aliyeahidwa[as] na kuwa katika Jumuiya yake. Siku itakuja ambapo mambo yote yatakuwa bayana kwao kwamba sisi Waislamu Waahmadiyya hatumkashifu wala kumtukana Mtume[saw] bali sisi ni wale wenye unyenyekevu na wenye kutoa huduma kwake zaidi kuliko watu wote duniani.

Khalifa Mtukufu[atba] alisema kwamba kwa hivyo, hatuwezi kuomba dhidi ya watu kama hawa, badala yake lazima tusaidie kuwaokoa kwa kuwaombea. Ahmadiyyat imeanzishwa kwa sababu ya kuwaokoa Waislamu. Tumepewa jukumu la kusaidia watu kufikia vilele vya juu, tunawezaje tena kuomba dhidi yao? Watu hawa wanaopotezwa watakapogundua ni kwa kiasi gani Waahmadiya wanampenda Mtukufu Mtume[saw], wao wenyewe watashuhudia kwamba Waahmadiya ndio watu ambao duniani wanasimamia heshima ya Mtukufu Mtume[saw]. Na hata tunaona kwamba wale ambao walikuwa wameathiriwa na wapinzani sasa wanatambua ukweli na wanakubali Ahmadiyyat.

Khalifa Mtukufu[atba] alisema kuwa kuna watu wengi ambao humwandikia barua wakisema kwamba wakati walipotafakari kwa dhati na kutafuta ukweli, mwishowe waliona nuru na sasa wanataka kukubali Ahmadiyyat. Hii imekuwa hivyo tangu wakati wa Masihi Aliyeahidiwa[as] na kwa Makhalifa wengine wote pia. Kwa hivyo, wakati wapinzani wanapopaza sauti zao na kuchukua hatua dhidi yetu, wanafanya kazi yetu kwa kueneza ujumbe wetu kwa njia ambazo labda sisi hatukuweza.

Khalifa Mtukufu[atba] alisema kuwa jukumu letu ni kuomba na kubaki wavumilivu. Hii ndio hatua bora zaidi ambayo itatuongoza kwenye mafanikio. Wajibu wetu ni kuwa na mawazo chanya na mioyo yetu tuiweke mbali na uovu wowote kwa Waislamu wengine. Lazima tuendelee kuomba ili Allah awawezeshe kuuona ukweli na wampokee Imam wa Zama haraka. Amin.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAMDH.-SHAW. 1442 AH | MEI 2021 | HIJRAT 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

"Mtu atakayeomba kama ilivyofundishwa katika Aya mbili za mwisho za Surat-ul-Baqara, basi zinamtosha" (Bukhari). Tena imesimuliwa, "Mtume^{saw}. alipoomba kwa maombi haya, akaambiwa katika kila tamko, 'Imefanywa'." Na Mtume^{saw}. akasema. "Allah Ameteremsha aya hizi mbili toka hazina za Peponi." (Baidhawi).

Kukabiliana na Mateso na Ukandamizaji kwa Maombi na Huruma

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 14/05/2020; Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu V, Hazrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad^{atba} ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz'); alisema kuwa katika siku za hivi karibuni, sheikh mmoja wa kisunni alikuwa akiongea kwenye mitandao ya kijamii kwamba ikiwa kuna machafuko yoyote duniani, ni kwa sababu ya ‹Makadiani›. Kwa hiyo kule katika nchi ya Palestina kunakotokea mauaji ya halaiki sababu yake pia ni Ahmadiyya.

Hii ndio njia na mbinu inayotumiwa na masheikh hawa wapinzani kueneza na kusambaza fitna na chuki dhidi ya Jumuiya duniani.

Na hii ni fadhila pakee ya Allah kwetu ya kwamba sisi tumepata bahati ya kumwamini Masihi Aliyeahidiwa^{as} ambaye ametupatia mafundisho kwamba uchochezi na fitna za aina hii tunapozisikia na kuziona sisi tusilipize kisasi. Badala yake tunatakiwa kuonesha subira na uvumilivu na kuwaombea kwa Allah msamaha na dua.

Ni 'Viongozi hawa wa upinzani' ambao wamewapotosha Waislam kwa jumla na ambao hawajui wema wowote katika kuwatendea Waahmadiyya ukatili. Walakini, maulamaa wale ambao wana ujuzi wanajua kuwa kile wanachosema hakina ukweli wowote; wanataka tu kuchochea fujo ili wadumishe nafasi zao kati ya watu.



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Khalifa Mtukufu^{atba} alisema kwamba Mungu anajua zaidi mwisho wao utakuwa nini; wajibu wetu sisi ni kuomba. Khalifa Mtukufu^{atba} alisema kwamba kama alivyosema katika hotuba yake ya Eid mapema siku hiyo, ni jukumu letu kuwaombea hata wapinzani wetu. Upinzani huu sio kitu kipya, bali umekuwa ukitokea tangu wakati wa Masihi Aliyeahidiwa^{as}.

Bali Masihi Aliyeahidiwa^{as} alikabiliwa na uadui na upinzani mkubwa na hata wale waliokuwa wanakuja kwake kusikiliza mafundisho yake pia walipata upinzani. Viongozi wa wapinzani wanataka kuwazuia watu wasiweze kusikiliza mafundisho mazuri ya Masihi Aliyeahidiwa^{as}. Kwa sababu wao wanajua wazi kama watu hawa watapata nafasi ya kusikiliza mafundisho yake lazima wataathirika nayo kwa sababu mafundisho yake ni ya kweli yanayotoka kwa Allah.

Khalifa mtukufu^{atba} anasema kazi yetu ni kuendelea kuomba dua. Mwisho wa siku ni kutoka katika watu hawa hawa watapatikana watu watakao kuwa na jazba na mapenzi kwa ajili ya Jamaat, nao mwishowe wataingia katika Jumuiya. Kwa hiyo sisi ni wajibu wetu kuendelea kuomba dua ili Allah atuondolee taabu hizi zinazotoka kwa watu hawa na awajaalie wao uongofu ili wajiunge na Jumuiya yake.

Tuendelee kuomba kila wakati, na kwa njia hiyo tutaeneza upendo ulimwenguni. Hata licha ya kusikiliza maneno makali yaliyosemwa juu yetu, tuendelee kuwaombea. Mungu Mwenyezi alimwambia Masihi Aliyeahidiwa^{as} kwamba matendo yao ni kwa sababu ya ukosefu wa uelewa na upendo wao potofu kwa Mtukufu Mtume^{saw} - ingawa wamepotoshwa, wanadai wanampenda. Kwa hivyo, Mungu Mwenyezi alimwamuru Masihi Aliyeahidiwa^{as} kwamba hapaswi kuomba dhidi yao, bali kinyume chake awaombee.

Khalifa mtukufu^{atba} baadae akanukuu maandishi ya Khalifa mtukufu wa Pili^{ra} yaliyohusu maisha ya Sayyedna Ahmad^{as} na jinsi alivyokabiliana na upinzani na uadui mbali mbali.

Hadhrat Muslih Maud^{ra} anasema mimi mwenyewe kwa macho yangu nimeshuhudia Masihi Aliyeahidiwa^{as} akifanyiwa uadui na upinzani mjini Lahore kwa kukashifiwa na kutukanwa kwa matusi mabaya na kashfa mbalimbali. Muda ule mimi nilikuwa na umri mdogo sikuweza

Endelea uk 11



KITABU

Ishara ya Kimbingu

Kitabu hiki, ambacho kimeandikwa na Hadhrat MIrza Ghulam Ahmad wa Qadian, ambaye amedai kuwa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi, aliyesubiriwa na dini zote kuu za dénia, kinarekodi shuhuda mbili za kiungu kuunga mkono madai yake.

Shuhuda zilitolewa na watakatifu wawili wa Kiislam kwa majina Gulab Shah na Nei'matullah Wali ambao waliishi muda mrefu kabla yake na walishuhudia ukweli wake katika mwanga wa funuo za kiroho walizopokea.

Hivyo, kitabu kinaangazia umuhimu wa shuhuda za kimbingu kwa dunia kumjua na kumtambua Imam na mteule wa kiroho wa zama. Kikiandikwa chini ya ufunuo wa kiungu, kitabu kitatia mvuto kwa wale ambao hutafuta mlinzi halisi wa ujumbe wa kiroho katika kila zama na wakati.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba ya Tsh· 3,000/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com